

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU



*Dar es Salaam*  
*21 Februari, 2025*

## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ametoa wito kwa wanawake waliobahatika kupata fursa ya elimu na kuwa viongozi kwenye maeneo mbalimbali kuhakikisha kuwa wanafanya kazi kwa bidii, weledi na uadilifu ili kuongeza imani na amani kwa jamii kuhusu umuhimu wa elimu kwa mtoto wa kike.

Rais Dkt. Samia ametoa wito huo leo kwenye maadhimisho ya miaka 10 tangu kuanza kwa Mafunzo ya Uongozi kwa Wanawake Tanzania (Female Future Program) sambamba na Mahafali ya Wahitimu wa Awamu ya 10 ya Mafunzo hayo na Mkutano wa 7 wa Uongozi, yaliyofanyika katika ukumbi wa The Super Dome.

Aidha, Rais Dkt. Samia amewataka wahitimu hao kuwa chachu ya maendeleo katika jamii na kutumia elimu na stadi za uongozi walizopata kunufaisha jamii kwa ujumla.

Vilevile, Rais Dkt. Samia amewarai wanawake kudhihirisha ushupavu wa uongozi kwenye Mashirika na Taasisi mbalimbali na kuwataka kuwa wabunifu kwenye kazi zao na kuwa waaminifu katika kulipa kodi ili kuwezesha utekelezaji wa miradi mbalimbali inayogusa maisha ya mwananchi.

Pia, katika kuhakikisha ustawi wa jamii, Rais Dkt. Samia amewahusia kuwa pamoja na elimu na nafasi za uongozi walizonazo, wasiache wajibu wao wa kijamii wa malezi na makuzi ya watoto ili kuwaepusha kujiingiza kwenye mienendo isiyofaa.

Kuhusu Uchaguzi Mkuu ujao, Rais Dkt. Samia amewahamasisha wanawake wenye sifa na uwezo kujiandikisha kupiga kura na kujitokeza kuwania nafasi mbalimbali.

Sharifa B. Nyanga  
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu



Ikulu Mawasiliano / ikulu\_mawasiliano /  
ikulu\_Tanzania / ikulu Tanzania /  
ikulumawasiliano / Ikulu Tanzania / Ikulu Tanzania



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU**



*Ikulu Mawasiliano / ikulu\_mawasiliano /  
ikulu\_Tanzania / ikulu Tanzania /  
ikulumawasilano / Ikulu Tanzania / Ikulu Tanzania*

